

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara Kuhusu Jinsi Chanjo za COVID-19 Hufanywa Nakala za Matokeo

Labda unasikia habari nyingi kuhusu chanjo za COVID-19 kwa sasa hivi. Tulitaka kujibu baadhi ya maswali ya kawaida kuhusu jinsi chanjo za COVID-19 zimetengenezwa.

Je, chanjo za COVID-19 hutengenezwaje kwa haraka zaidi?

Kawaida, kujaribu chanjo ili kuhakikisha ni salama na inafanya kazi hufanywa kabla ya kutengeneza kiasi kingi cha chanjo. Kwa sababu ya janga na pesa kutoka kwa serikali kuu, wanasayansi walifanya hatua hizi zote kwa wakati mmoja. Ni chanjo tu ambazo zimejaribiwa na kuonyeshwa kuwa ni salama ndizo zinazotumiwa.

Je, chanjo za COVID-19 hujaribiwaje?

Chanjo zote za COVID-19 hupitia vipimo vinavyoitwa majaribio ya kimatibabu. Kila chanjo hupitia zaidi ya kipimo kimoja. Kwanza, chanjo hupimwa katika kundi ndogo ya wanaojitolea, kisha kundi la mamia ya watu, kisha kumi ya maelfu ya watu. Wanaojitolea kufanya majaribio ya chanjo ya COVID-19 hutoka jamii na asili nyingi tofauti. Huu ndio mchakato unaotumiwa kufanya majaribio ya chanjo zingine.

Je, chanjo za COVID-19 huidhinishwaje?

Kwa chanjo zinazopita vipimo vyote, timu ya wataalam wa kimatibabu wataangalia matokeo ya kipimo na vile watu walihisi baada ya kupewa chanjo. Ikiwa chanjo inafanya kazi na ni salama, huwa inaidhinishwa. Kuna makundi mengi ya wanasayansi na wataalam ambao wanakagua data ya usalama wa chanjo ya COVID-19 na kufanya mapendekezo. Chanjo zile zimeidhinishwa ndizo tu zinazopewa watu.

Je, ni nani anapata chanjo wa kwanza?

Kundi la ushauri la kitaifa la CDC liliangalia data na likafanya mapendekezo ya yule anapaswa kupewa chanjo kwanza. Makundi mengine ambayo yako katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa COVID-19 au wanaweza kuwa wagonjwa zaidi kutokana na COVID-19, walipata chanjo wa kwanza. Minnesota ina timu ya wataalam ambao watasaidia kuhakikisha kuwa chanjo inapatikana kwa kila mtu kwa njia ya haki, ikiangazia usawa wa afya. Chanjo nyingi zinapoendelea kupatikana wakati unaposonga, watu zaidi watapata kuchanjwa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu chanjo ya COVID-19 tembelea tovuti ya idara ya afya.

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

2/9/21 (Swahili)

Ili kupata maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu kwa: 651-201-4989.